# Tanzania

## Taarifa ya Maendeleo ya Uhuru na Demokrasia - 2008.
**Imetolewa na ofisi ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi. Mei 23, 2008.**

**Sehemu ya kwanza.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina Rais ambaye ni mkuu wa Serikali na Bunge. Mwezi Desemba mwaka 2005 katika uchaguzi wa Rais na wabunge, wananchi wa Tanzania walimchagua Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais na Chama cha Mapinduzi ambacho ni chama tawala, kilijipatia viti vingi bungeni. Waangalizi wa uchaguzi waliuchukulia uchaguzi huo kwa kiasi kikubwa kwamba ulikuwa wa haki na huru. Kisiwa cha Zanzibar, ingawa ni sehemu ya Muungano kimuundo wa kiserikali na chama, kina Rais wake, mfumo wake wa mahakama na Bunge, kinaendelea kujiendesha chenyewe kwa kiasi kikubwa. Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar mwaka 2005, ulikuwa na dosari nyingi na vurugu zilizochochewa kisiasa katika maeneo ya mjini. Rekodi ya jumla ya Serikali juu ya haki za binadamu si ya kuridhisha, ingawa kuna maendeleo katika uhuru wa vyombo vya habari kwa upande wa Tanzania bara. Matatizo ya haki za binadamu yameendelea kuongezeka. Polisi na askari wa magereza wamekuwa wakitumia nguvu nyingi dhidi ya watuhumiwa na wafungwa hadi wakati mwingine kusababisha vifo, polisi kushindwa kuwajibika limekuwa ni tatizo, taarifa zimekuwa zikiendelea kutolewa juu ya mauaji ya vikongwe wanaotuhumiwa kwa uchawi, hali ya magereza imeendelea kuwa mbaya na ya kutishia maisha, kumekuwa na tuhuma nyingi za rushwa kwa polisi na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kisheria, mahakama zimekithiri kwa rushwa na utendaji usio na ufanisi hasa katika mahakama za ngazi za chini; uhuru wa kujieleza na wa habari kwa kiasi fulani umekuwa finyu, rushwa Serikalini imezidi kuenea, unyanyasaji dhidi ya wanawake umekuwa ukiendelea, na usafirishaji haramu wa binadamu na utumikishaji wa watoto bado ni tatizo.

**Sehemu ya pili.**

Katika mwaka wa 2007, vipaumbele na taarifa mbalimbali za Serikali ya Marekani zimekuwa ni za kutetea na kusisitiza misingi ya demokrasia katika kutilia mkazo uhuru wa vyombo vya habari na kusaidia juhudi za Serikali katika kujenga Serikali imara, yenye kuwajibika, inayowakilisha wengi na yenye kuhimiza ujenzi wa taasisi zinazoendeleza utawala wa sheria na demokrasia ya walio wengi. Kufanikisha mkakati huu, Serikali ya Marekani imesaidia juhudi za Serikali katika kupunguza rushwa kwa kutoa mafunzo na kusaidia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kipaumbele kwa Watendaji wa Ubalozi ni kuimarisha mipango inayosimamiwa na Serikali ya Marekani na Asasi za kiraia zinazohimiza uhuru wa vyombo vya habari na uandishi wa habari za kichunguzi, kuongeza usimamizi na uhuru wa Bunge, na kuyawezesha mashirika ya ndani yasiyo ya Kiserikali kuweza kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali.

**Sehemu ya tatu.**

Serikali ya Marekani itaendelea kutetea na kuendeleza demokrasia kupitia njia mbalimbali za kidemokrasia. Katika mwaka wote wa 2007 Balozi na watendaji wengine Ubalozini wamekuwa wakisisitiza hadharani kwamba uhuru wa vyombo vya habari ni msingi wa kukua kwa demokrasia nchini. Balozi alisema katika Chuo cha Uandishi wa habari na kuidhinisha kwamba misaada itolewe kwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotetea na kulinda uhuru wa vyombo vya habari. Alimteua mmiliki mmoja mkubwa wa vyombo vya habari aliyewaunga mkono wahariri na waandishi wake katika habari zao za kichunguzi kuwa mtunukiwa wa tuzo ya siku ya Martin Luther King ifanyikayo Ubalozini kila mwaka. Balozi pia amewahimiza maofisa wote Ubalozini kuwatunukia vyeti maafisa wa mradi wa mfumo wa kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali, waliofanya kazi kwa umakini kutekeleza programu za uwajibikaji katika vijiji vyao.

Marekani imesaidia kutoa elimu ya uraia, ikiwemo kutoa mafunzo ya elimu ya kiraia kwa vikundi mbalimbali vya kijamii katika jamii ya Waswahili wa Pwani na kwa akina Mama wa Kimasai ili kuongeza ushiriki wao katika mchakato wa demokrasia. Huko kisiwani Pemba, mkakati wa juhudi mpya za maafikiano ulizinduliwa kati ya akina Mama wa vyama pinzani vya siasa. Mashirika yote yalio chini ya Ubalozi yameanzisha miradi ili kuyafikia makundi ya dini ili kuongeza fursa za majadiliano kwa makundi yenye imani tofauti.

Serikali ya Marekani imetoa mchango mkubwa katika juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha uwezo wa Serikali, mfumo wa sheria ili kuweza kuziendesha kesi za rushwa. Juhudi za mwaka mzima za Serikali ya Marekani, zimekuwa ni kichocheo kikubwa katika upitishwaji na utekelezaji wa sheria za usafirishaji fedha kwa njia haramu, ambayo ni hatua muhimu katika kujenga kikosi maalum cha kupambana na uhalifu wa kifedha. Kuboresha mazingira ya sheria ili kuzishughulikia kesi za rushwa, Marekani iliandaa warsha kwa waandishi wa habari na maofisa wa Serikali juu ya umuhimu wa kuwalinda watoaji taarifa za rushwa. Serikali pia imesaidia juhudi za Rais Kikwete kuiimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Taasisi ya Millenium Challenge imetoa mafunzo kwa mahakimu 30 juu ya sheria dhidi ya rushwa na jinsi ya kuitumia vizuri mahakamani. Ikishirikiana na mashirika ya kiraia, Serikali ya Marekani imetekeleza mifumo 11 ya kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali wilayani Tanzania nzima. Mifumo hii ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma, imewawezesha wananchi kuiwajibisha Serikali yao kutoa huduma kwa umma. Mnamo mwezi Agosti mwaka 2007, hotuba ya Balozi aliyoitoa katika sherehe za TAKUKURU iliibua mjadala wa kitaifa juu ya majukumu ya nchi wafadhili kwamba ni kuifanya Serikali iwajibike zaidi.

Serikali ya Marekani imesaidia kuboresha mfumo wa ununuzi wa mali ya umma nchini na kuihimiza Mamlaka ya Uthibiti wa Manunuzi kujenga utamaduni wa

kuweka taarifa zake hadharani. Moja ya taarifa hizo iliifikia kamati muhimu ya Bunge iliyokuwa ikichunguza taratibu za ununuzi katika shirika la umma la umeme Tanesco. Mapema mwaka 2008 ripoti ya kamati iligundua kwamba Waziri Mkuu na waziri mwingine Serikalini waliingilia baadhi ya taratibu za ununuzi. Muda mfupi baadaye Waziri Mkuu ilibidi ajiuzuru na baadaye mabadiliko makubwa ya baraza la mawaziri yalifuata. Ripoti ya kamati pia ilishauri uimarishwaji wa Bunge ili wabunge waanze kuchukua nafasi za kuwa chombo cha kuangalia utendaji wa Serikali kuu.

**Sehemu ya nne**

Serikali ya Marekani imesaidia kuboresha mfumo wa sheria kwa kuanzisha mtandao wa msaada wa kisheria ili kuongeza upatikanaji wa haki kwa watu walio na kipato cha chini vijijini. Serikali ya Marekani imeendelea kutoa mafunzo kwa jeshi la polisi juu ya namna ya kudhibiti machafuko ya kiraia ili kuwajengea uwezo polisi wa kuweza kumudu maandamano ya amani na mikusanyiko mingine mikubwa.

Serikali ya Marekani pia imetoa mafunzo kwa kuwafundisha akina Mama wa Kimasai juu ya haki zao, ikiwa ni pamoja na kuachana na tabia ya ukeketaji kwa wanawake. Marekani imefanya kazi na maofisa wa Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kimataifa kujenga ufahamu juu ya usafirishaji haramu wa binadamu na kuwachukulia hatua za kisheria wanaofanya biashara hiyo. Kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti 2007, Marekani imetoa mafunzo juu ya usafirishaji haramu wa binadamu na msaada wa kiufundi kwa polisi na maofisa uhamiaji bara na visiwani, kwa waendesha mashtaka na mahakimu. Mpango huu ulibuniwa kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na kuwalinda waathirika wa tatizo hili. Pia, Marekani imesaidia kujenga sehemu tatu za makazi kwa waathirika wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu. Warsha ya kujenga ufahamu juu masuala ya VVU/UKIMWI iliyofanyika mjini Dodoma imesaidia kupambana na ubaguzi dhidi ya wanaoishi na VVU na UKIMWI.

## Mwisho